# Waanzisha kampeni kusaidia wenye ugonjwa wa akili Dar

SUNDAY MAY 30 2021

(https://twitter.com/share?text=Waanzisha kampeni kusaidia wenye ugonjwa wa akili Dar&url=https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/k kampeni-kusaidia-wenye-ugonjwa-wa-akili-dar-3419126&via=MwananchiNews) (https://www.facebook.com/sharer.php?u=https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/ kampeni-kusaidia-wenye-ugonjwa-wa-akili-dar-3419126) in (https://www.linkedin.com/shareArticle?mini=true&url=https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/waanzisha-kampeni-kusaidia-wenye-ugonjwa-wa-akili-dar-3419126) (mailto:?subject=Waanzisha kampeni kusaidia wenye ugonjwa wa akili Dar&body=Waanzisha kampeni kusaidia wenye ugonjwa wa akili Dar-https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/waanzisha-kampeni-kusaidia-wenye-ugonjwa-wa-akili-dar-3419126)




**Summary**

- **Asasi ya Tap Elderly Women's Wisdom For Youth (TEWWY) imeanzisha kampeni ya kuhamasisha wananchi kuhusu afya ya akili katika mitaa 15 jijini Dar es Salaam ikiwa ni juhudi za kuhamasisha watu kutambua afya zao.**

ADVERTISEMENT



**By Elias Msuya**
More by this Author (/mw/elias-msuya-2872238)

Dar es Salaam. Wakati ikielezwa kuwepo kwa ongezeko la watu wanaougua ugonjwa wa akili, asasi ya Tap Elderly Women's Wisdom For Youth (TEWWY) imeanzisha kampeni ya kuhamasisha wananchi kuhusu afya ya akili katika mitaa 15 jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa mradi huo, ofisa wa asasi hiyo, Morris Lekule alisema mradi huo uliofadhiliwa na taariri ya GivenGain (GG) kupitia One In An Amry (OIAA) utatekelezwa katika kata moja kila Manispaa na mitaa mitatu kila kata itakayochaguliwa jijini Dar es Salaam.

Uchangiaji hujumuisha michango midogo midogo kuanzia dola moja na kuendelea. Michango yato kwenye jukwaa hili walifanikiwa kupata $19,000.00

"TEWWY imewezesha mafunzo ya kwa wanasihi saba wapya kuongezea katika 11 waliopo sasa, ambao wataendesha kipindi kimoja cha unasihi kila wiki kwa wiki 15 ktk kila mtaa," alisema Lekule.

Pia alisema kutakuwa na uwekaji wa mabango yatawekwa kwenye mitaa iliyochaguliwa kuhamasisha jamii kushiriki vipindi vya unasihi kila wiki.

Alizitaja manispaa zitakazohusishwa kluwa pamoja na Ilala itakayokuwa na mitaa ya Tabata,Tabata Msimbazi, wakati katika manispaa ya Kigamboni kutakuwa na kata za Kigamboni na Somanga na mitaa ya Twamoyo, Kizani na Mwela.

ADVERTISEMENT

Katika Manispaa ya Kinondoni kutakuwa na kata ya Kawe na mitaa ya Ukwamani, Mbezi beach A na Mzimuni, wakati Manispaa ya Temeke itakuwa na kata ya Mbagala na mitaa ya Manygaya, Kizinga na Mbagala, huku Manispaa ya Ubungo ikiwa na mitaa ya Kibo, NHC na Kisiwani.

Katika utekelezaji wa mradi huo, Pia Lekule alisema wanasihi watawashauri wateja wote wenye matatizo yaliyo na viashiria vya magonjwa kwenda vituo vya afya vilivyo kwenye manispa zao.

Alizitaja dalili za ugonjwa wa akili kuwa pamoja na msongo uliopitiliza na sonona baada ya kufanyiwa kipimo, Skizofrenia na baipola

Akieleza ukubwa wa tatizo wa magonjw aya akili, Mkurugenzi wa TEWWY, Rustika Tembele alisema tatizo hilo linaongezeka duniani.

“Shirika la Afya Duniani lina tahadharisha kwamba ifikapo 2030 Sonona inaweza ikawa mojawapo ya mchangiaji mkubwa wa matatizo ya afya ya akili Duniani,” alisema Tembele.

Mbaya zaidi alisema wahudumu wa afya ya akili hawatoshi, kwani katika Afrika kuna chini ya Daktari mmoja wa magonjwa ya akili kwa kila watu 100,000!

ADVERTISEMENT

## Habari kuu

## Profesa Mbarawa aanza na Tanroads (/mw/habari/kitaifa/profesa-mbarawa-aanza-na-tanroads--3549054)



(/mw/habari/kitaifa/profesa-mbarawa-aanza-na-tanroads--3549054)

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Profesa Makame Mbarawa ameanza kazi kwa kuitaka Wakala wa Barabara Nchini (Tanroads) kutafuta kifaa cha kupimia...

## Rais Samia kuhusu uteuzi wa Dk Tax kwenda Wizara ya Ulinzi (/mw/habari/kitaifa/rais-samia-kuhusu-uteuzi-wa-dk-tax-kwenda-wizara-ya-ulinzi-3548558)



(/mw/habari/kitaifa/rais-samia-kuhusu-uteuzi-wa-dk-tax-kwenda-wizara-ya-ulinzi-3548558)

Rais Samia Suluhu Hassan amesema katika mabadiliko aliyofanya ameamua kuvunja ile dhana ya muda mrefu kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga...

Samia afyeka mawaziri watatu, ateua wapya watatu (/mw/habari/kitaifa/samia-afyeka-mawaziri-watatu-ateua-wapya-watatu-3548038)

Rais Samia: Tuendako Serikali itaendeshwa kwa matendo makali (/mw/habari/kitaifa/rais-samia-tuendako-serikali-itaendeshwa-kwa-matendo-makali-3548918)

Rais Samia ataka wakuu wa mikoa kuwatafutia maeneo ya biashara wamachinga (/mw/habari/kitaifa/rais-samia-ataka-wakuu-wa-mikoa-kuwatafutia-maeneo-ya-biashara-wamachinga-3548956)

Jeshi la Polisi latia mguu shule za dini (/mw/habari/kitaifa/jeshi-la-polisi-latia-mguu-shule-za-dini-3547932)

Wachambuzi wanavyozungumzia uteuzi wa Rais Samia (/mw/habari/kitaifa/wachambuzi-wanavyozungumzia-uteuzi-wa-rais-samia-3548494)

**HABARI ZAIDI**

(/Mw/Habari)

Biashara (/Mw/Habari/Biashara)

Makala (/Mw/Habari/Makala)

**MICHEZO**

(/Mw/Michezo)

Burudani (/Mw/Michezo/Burudani)

**PICHA**

(/Mw/Picha)

**VIDEO**

**TOLEO MAALUM**

(/Mw/Video)

(/Mw/Toleo-Maalum)

**AJIRA**

(/Mw/Ajira)

**NOTISI**

(/Mw/Notisi)

Zabuni (/Mw/Notisi/Zabuni)

MWANANCHI (/mw)

**Apps**

(https://play.google.com/store/apps/develop
id=Nation%20Media%20Group&hl=en&
Other-global-all-co-prtnr-py-PartBadge-Mar2515-1)

(https://itunes.apple.com/us/developer/natio
media-group-ltd/id771736036)

**Information**

Contact Us (https://nation.africa/kenya/cont
us-294088)

Frequently asked questions (https://nation.africa/kenya/freq
asked-questions-303716)

NMG Privacy Policy (https://nation.africa/kenya/nmg
privacy-policy-303724)

Terms of use (https://nation.africa/kenya/term
of-use-303726)

Terms and Conditions of Use (https://nation.africa/kenya/term
and-conditions)

Our Blog Rules (https://nation.africa/kenya/our-blog-rules-549010)

**NMG Sites**

E-Papers (https://newsstand.nationmedia.com)
Business Daily (http://www.businessdailyafrica.com/)
Daily Monitor (http://www.monitor.co.ug/)
Mwananchi (https://www.mwananchi.co.tz/)
Mwanaspoti (http://www.mwanaspoti.co.tz/)
Taifaleo (http://taifaleo.nation.co.ke/)
Swahilihub (http://www.swahilihub.com/)
The Eastafrican (http://www.theeastafrican.co.ke/)
Nation Media Group (http://www.nationmedia.com/)

**Tufuate**

(https://www.youtube.com/user/mcl992) (https://twitter.com/MwananchiNews)

(/service/rss/mw/2739162/feed.rss)
(https://www.facebook.com/MwananchiNews)
(https://www.instagram.com/mwananchi_official/)